**THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL**
**Kenya Primary School Education Assessment**

# KISWAHILI

**602**

## LUGHA

## Nov. 2022 – Muda: Saa 1

### MAAGIZO KWA WATAHINIWA (Soma maagizo yafuatayo kwa makini)

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 30. Jibu maswali yote.
2. Ukiisha kuchagua jibu lako, lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

### JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

3. Tumia penseli ya kawaida.
4. Hakikisha ya kwamba karatasi ya majibu uliyopewa imejumuisha yafuatayo:

   **NAMBA YAKO YA TATHMINI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**
   **JINA LA SOMMO**

5. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
6. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
7. Kwa kila swali 1–30 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
8. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

   **Mfano:**
   **Katika kijitabu cha maswali:**

   **28.** Maneno katika jedwali hili yanastahili kuwa katika hali ya umoja pekee. Chagua jibu lenye maneno yasiyo katika hali ya umoja.
   A. yai, dirisha, chandarua
   B. uso, msusi, mwiko
   C. ufagio, kiti, mswaki
   D. kuni, vifutio, matunda

   Jibu sahihi ni D.

   **Katika karatasi ya majibu:**

   28 [A] [B] [C] [D]

   Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba **28**, kisanduku chenye herufi D ndicho kilichochorwa kistari.

9. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
10. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

934

A447

KPSEA 2022

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 4 zilizopigwa chapa.**

*© 2022 The Kenya National Examinations Council*



318957

**Geuza ukurasa**

**Swali la 1 hadi la 5.**

*Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali.*

*(Babu ameketi chini ya mti akisoma gazeti. Analiweka gazeti kando anapomwona Muli)*

Muli: *(akimsogelea Babu)* Shikamoo Babu?

Babu: *(kwa tabasamu)* Marahaba mjukuu wangu! Habari za shule?

Muli: Njema babu! *(kimya)* Babu, nikwambie kitu?

Babu: Naam, niambie mjukuu wangu.

Muli: Wenzangu walinichagua kuwa kiranja wa darasa.

Babu: Hongera! Jambo zuri.

Muli: *(akijikuna kichwa)* Lakini Babu, sijui ninastahili kufanya nini ili niwe kiongozi bora.

Babu: Aha! Muli, sikiliza, ili kuwa kiongozi bora unastahili kuwa na maadili.

Muli: Ooh! Maadili ...

Babu: Naam mjukuu wangu. Unaweza kuonyesha **maadili** kwa namna mbalimbali. Kwanza uwahudumie wenzako bila kuwabagua.

Muli: Kweli Babu, ninafikiria pia ninastahili kuwaonyesha upendo.

Babu: Ndiyo Muli. Unaweza kufanya hivyo kwa kuwajali na kuwasaidia wenzako.

Muli: Kweli Babu! Ninaona kwamba heshima, umoja na ushirikiano pia ni mambo muhimu.

Babu: Haswa! Heshima si utumwa. Je, unaweza kuonyesha heshima kwa njia gani?

Muli: *(Kwa ujasiri)* Kwa kuwaamkua wote na kusikiliza wanayoyasema.

Babu: Vyema! Unastahili pia kuwa mwaminifu. Tunaonyesha uaminifu kwa kusema ukweli na kufanya mambo inavyostahili.

Muli: Asante babu! Hakika umenifunza mengi.

**1.** Muli alipoulizwa na babu kuhusu habari za shule, alimjibu
A. Naam
B. Njema
C. Shikamoo
D. Marahaba

**2.** Maneno yafuatayo yametumiwa katika mazungumzo. Lipi **halionyeshi** adabu?
A. Karibu
B. Naam
C. Asante
D. Kweli

**3.** Ni jibu lipi linaloonyesha maadili ambayo Babu alimfunza Muli?
A. Kuhudumia, kuheshimu na kusikiliza.
B. Kuamkua, kusikiliza na kujali.
C. Kujali, kusaidia na kuwa mwaminifu.
D. Kuwa na heshima, kushirikiana na kusaidia.

**4.** Unafikiri Muli atafanya nini baada ya kumuaga Babu?
A. Atafurahia kuwa kiongozi shuleni.
B. Atazingatia mawaidha ya babu.
C. Atawaeleza wenzake kuhusu alivyokutana na babu.
D. Atawapongeza wenzake kwa kumchagua kuwa kiranja

**5.** Neno **maadili** limetumika katika mazungumzo maana yake ni
A. Mienendo mizuri inayofaa kuzingatiwa na mtu.
B. Maonyo ambayo hutolewa mtu anapokosea.
C. Matendo ambayo mtu huwafanyia wenzake.
D. Mitindo mipya inayofuatwa na mtu.

**Swali la 6 hadi la 9**
*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Sungura alirauka kabla ya jua kuchomoza. Alianza safari ya kwenda kumtembelea shangazi yake. Njiani alipanda milima na kuvuka mabonde. Jua lilipochomoza, aligundua kuwa alikuwa ametembea sana ila hakuwa amefika kwa shangazi yake. Alikuwa anaelekea kusini badala ya kaskazini. Kumbe alikuwa amepotea njia!

"Nitafanya nini? Nimepotea njia," Sungura alijisemea kwa sauti.

"Nitakusaidia," alisema Kobe aliyekuwa kichakani, hapo karibu.

"Asante sana Kobe. Sikuwa nimekuona. Tafadhali nisaidie," Sungura alimwomba Kobe.

"Unakwenda upande gani?" Kobe alimuuliza Sungura.

"Naelekea kaskazini, anakoishi shangazi yangu," Sungura alimjibu Kobe.

"Jua huchomoza upande wa Mashariki wa dira kila asubuhi. Ukitaka kwenda Kaskazini, simama kisha unyooshe mikono yako juu. Mkono wa kulia uelekeze kunakotoka jua. Huko ndiko Mashariki. Nao mkono wa kushoto uelekeze upande huo mwingine. Huko ndiko Magharibi," Kobe alimweleza Sungura huku akimwonyesha kwa vitendo.

"Kwa hivyo uso wangu utakuwa unaangalia Kaskazini huku mgongo wangu ukiwa upande wa Kusini" Sungura alisema kwa furaha.

"Wewe ni mwanafunzi mzuri. Unaelewa haraka. Umelenga ndipo," Kobe alimwambia Sungura kwa bashasha.

"Undugu ni kufaana. Asante sana Kobe," Sungura aligeuka akarudi hadi kwake ili kuanza safari upya.

**6.** Nyumbani kwa Shangazi kulikuwa upande gani kutoka kwa Sungura?
A. Mashariki
B. Magharibi
C. Kaskazini
D. Kusini

**7.** Kwa nini Sungura aliamka mapema? Ili
A. apande milima na kuvuka mabonde.
B. aone jua likichomoza.
C. akutane na Kobe njiani.
D. aende kumtembelea Shangazi.

**8.** Kobe anawajali wengine. Chagua jibu linaloonyesha sifa hii ya Kobe.
A. Alimwelekeza Sungura alikokuwa akienda.
B. Anamsikiliza Sungura akizungumza.
C. Alikubali zawadi alizopewa na Shangazi.
D. Alifikiria Sungura alikuwa mwanafunzi mwerevu.

**9.** Chagua jibu lenye neno ambalo Shangazi angetumia kumwita Sungura.
A. Binamu
B. Mpwa
C. Ndugu
D. Ami

**Swali la 10 hadi la 12**
*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Shule ya msingi ya Faulu huwa na siku tatu za michezo katika kila juma. Wanafunzi wa Gredi ya Sita wamegawanywa katika vikundi vinne kama ifuatavyo:

Simba Kifaru Chui Ndovu

Kila kikundi hushiriki katika michezo tofauti kila juma. Tazama jedwali la juma hili kisha ujibu maswali.

| VIKUNDI | JUMATATU | JUMATANO | IJUMAA |
|---|---|---|---|
| Simba | Kandanda | Netiboli | Riadha |
| Kifaru | Riadha | Uogeleaji | Kandanda |
| Chui | Netiboli | Riadha | Uogeleaji |
| Ndovu | Uogeleaji | Kandanda | Netiboli |

**10.** Ni kikundi kipi hakikushiriki kandanda?
A. Simba
B. Chui
C. Kifaru
D. Ndovu

**11.** Ni kikundi kipi hakikushiriki uogeleaji?
A. Ndovu
B. Kifaru
C. Chui
D. Simba

**12.** Ni kikundi kipi hakikushiriki riadha?
A. Simba
B. Chui
C. Ndovu
D. Kifaru

**Swali la 13 hadi la 15**
*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali*

Je, unajua kupika ugali? Kupika ugali ni rahisi. Kwanza, unahitaji unga wa mahindi, maji, sufuria, mwiko na jiko la kupikia lenye moto. Anza kwa kupima kiasi cha maji unayohitaji na kuyatia kwenye sufuria safi. Ibandike sufuria hiyo kwenye jiko. Funika sufuria ili uyapatie maji muda yachemke. Chukua unga kisha uutie kidogo kidogo ndani ya maji yanayochemka, huku ukikoroga kwa mwiko. Ongeza unga kulingana na unavyotaka ugali wako uwe. Kama unataka ugali mgumu, basi endelea kuongeza unga. Funika ugali wako, kisha upunguze moto jikoni ili ugali uive polepole.

Unaweza kuandaa ugali kwa vitoweo vya aina mbalimbali. Kuna wale wanaopenda kula ugali kwa maziwa yaliyoganda na mboga za kienyeji kama vile mchicha. Wengine hula ugali kwa samaki au nyama. Mimi napenda kula ugali kwa dagaa na kachumbari. Je, wewe unapenda kula ugali kwa kitoweo gani?

**13.** Wewe unajiandaa kupika ugali.
Chagua jibu linaloonyesha hatua ya kwanza utakayozingatia.
A. Kuwa na vitu utakavyohitaji kupika ugali.
B. Kuinjika sufuria yenye maji jikoni.
C. Kuchukua mwiko na kuanza kukoroga.
D. Kuwa na kitoweo ambacho unahitaji.

**14.** Unampikia nyanya kitoweo cha kuliwa kwa ugali.
Chagua jibu linaloonyesha kitoweo chenye lishe bora.
A. Nyama na dagaa.
B. Kabeji na sukumawiki.
C. Samaki na mboga ya mchicha.
D. Maziwa na maharagwe.

**15.** Chagua jibu sahihi.
Mchicha huupatia mwili vitamini, ugali huupatia mwili______
A. protini.
B. madini.
C. kinga.
D. wanga.

*Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi **16** hadi **20**. Umepewa majibu **manne** hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.*

Kanini **16** katika michezo mbalimbali tukiwa shuleni. Mchezo **17** alipenda zaidi ni netiboli. **18** na timu ya mchezo wa netiboli **19** alipoingia darasa la tano. Kanini alitia bidii kwenye mchezo huu na kuiletea timu yake ushindi. Alifahamu kuwa **20**.

**16.** A. alishirikia
B. alishiriki
C. alishirikisha
D. alishirikiwa

**17.** A. ambao
B. ambayo
C. ambako
D. ambamo

**18.** A. Alikuunga
B. Aliwaunga
C. Alijiunga
D. Alituunga

**19.** A. huku
B. kama
C. tena
D. mara

**20.** A. kila mwamba ngoma ngozi huivuta kwake
B. mtaka cha mvunguni sharti ainame
C. udongo upatilize uli maji
D. jifya moja haliinyiki chungu

*Kutoka swali la 21 hadi la 30, chagua jibu sahihi.*

**21.** Wanafunzi wana nidhamu, ________ huheshimu walimu.
A. wao
B. wewe
C. yeye
D. nyinyi

**22.** Tunasema, wingu ni kwa nzige. Tutasema, _________ ni kwa matunda.
A. kitia
B. pakacha
C. bunda
D. robota

**23.** Chagua wingi wa:
Fundi yule hodari amejenga ukuta mrefu.
A. Mafundi wale hodari wamejenga kuta ndefu.
B. Fundi wale hodari wamejenga ukuta mrefu.
C. Mafundi wale hodari wamejenga ukuta mrefu.
D. Fundi wale hodari wamejenga ukuta mrefu.

**24.** Kimeto alimsaidia Kamaa kuchora picha. Kamaa alikuwa ameumia mkono. Kwa hivyo, Kimeto
A. alimchoresha Kamaa picha.
B. alimchorea Kamaa picha.
C. alichoreshwa picha na Kamaa.
D. alichoreshea Kamaa picha.

**25.** Ni sentensi ipi **sahihi**?
A. Palipo na rutuba panafaa kwa kilimo.
B. Palipo na rutuba kunafaa kwa kilimo.
C. Mlimo na rutuba panafaa kwa kilimo.
D. Mlimo na rutuba kunafaa kwa kilimo.

**26.** Ni sentensi ipi iliyoafikishwa vyema?
A. Neema amefika: kwetu leo asubuhi.
B. Mwachia amenunua machungwa, maembe na papai.
C. Je, umeandika barua ya kuomba msamaha.
D. Salaale Kalama amefunga bao lingine.

**27.** Chagua ukubwa wa sentensi ifuatayo:
Mlango wa nyumba yake unapendeza.
A. Lango la jumba lake linapendeza.
B. Mlango wa jumba lake linapendeza.
C. Lango la nyumba yake linapendeza.
D. Mlango wa nyumba yake linapendeza.

**28.** Chagua jibu **lisilo** sahihi.
A. Tita la kuni.
B. Thureya ya nyota.
C. Kicha cha funguo.
D. Kilinge cha wanariadha.

**29.** Tunastahili kupiga chafya kwenye kiwiko cha mkono. Kupiga chafya ni
A. kuchemua.
B. kukohoa.
C. kutema.
D. kupenga.

**30.** Simon ni wembe masomoni. Kauli hii ina maana kuwa Simon ni:
A. mwenye subira.
B. jasiri.
C. mwenye bidii.
D. mwerevu.

934

A447